# HOTUBA YA NDUGU GODFRED B. MBANYI MKURUGENZI MTENDAJI WA BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI (PSPTB) KATIKA MAHAFALI YA 14 YA PSPTB JUMAMOSI, TAREHE 25 OKTOBA, 2025.

Ndugu Dkt. Natu El-maamry Mwamba – Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mgeni Rasmi kwenye mahafali ya 14 ya PSPTB,

Ndugu Dkt Frederick A. Mwakibinga- Kamishina wa Sera ya Ununuzi - Wizara ya Fedha,

Ndugu Bw. Jacob Jail Kibona - Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi PSPTB,

Ndugu Wakurugenzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB,

Ndugu Wakuu wa taasisi na viongozi mbalimbali waalikwa,

Ndugu Wafanyakazi wa Bodi,

Ndugu Wahitimu wote,

Ndugu Wageni waalikwa,

Ndugu Wanahabari,

Mabibi na Mabwana,

**ITIFAKI IMEZINGATIWA.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Awali ya yote, nitoe shukrani zangu za dhati kwako kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wataalam wa fani ya ununuzi na ugavi kwa kukubali kwako mwaliko wetu wa kuja kujumuika nasi katika mahafali ya 14 ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) kama Mgeni Rasmi na Mlezi wa fani hii ya Ununuzi na Ugavi nchini.

Tunatambua una majukumu mengi ya Kiwizara na Kitaifa, lakini hata hivyo umeweza kutenga muda na kuungana nasi kwenye mahafali haya. Hii inaonyesha ni kwa jinsi gani unajali taaluma hii ya ununuzi na ugavi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Kwa ruhusa yako, niwashukuru na kuwakaribisha wadau na wageni wetu wote waliofika kuhudhuria mahafali haya ambapo wahitimu mbalimbali katika fani ya Ununuzi na Ugavi, watatunukiwa vyeti vyao na wewe Mgeni Rasmi. Napenda kusema karibuni sana katika shughuli hii.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Dira ya Bodi hii, ni kuwa ubora katika utendaji wa mnyororo wa Ununuzi na Ugavi yaani “*Excellency in Procurement and Supply chain Practices’’*. Ili kufanikisha adhima hii, Bodi ina wajibu wa kutoa maarifa na ujuzi unaozingatia umahili katika utendaji wa mnyororo wa ununuzi na ugavi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Hili linatekelezwa kupitia mtaala unaotumika katika mafunzo ya kitaaluma yanayopelekea kuwapima watahiniwa kupitia mitihani ya Kitaaluma. Katika mahafali haya wako wahitimu **368** katika ngazi tatu na watatunukiwa vyeti vya Stashahada ya kitaaluma yaani “*Professional Diploma in Procurement and Supply management’’* ***wapo 20***, Shashahada ya kitaaluma (*Graduate Professional in Procurement and Supply Management)* **wapo 44** na shahada ya juu kitaaluma yaani ‘’*Certified Procurement and Supply Professional-Tanzania’’* (CPSP-T) **wapo 304**. Wahitimu hawa walifaulu mitihani ya kitaaluma iliyofanyika mwezi Novemba, 2024, Mwezi Mei 2025 na Agosti, 2025 katika ngazi zote tatu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Vile vile Bodi iliendesha mafunzo ya ukaguzi kwa wataalam wa Ununuzi na Ugavi watakaotumika katika kusaidia ukaguzi katika eneo la utendaji wa mnyororo wa ununuzi na ugavi ikiwemo miradi na hata kaguzi maalum. Jumla ya wahitimu 131 wako katika mahafali hii ili kupokea vyeti vyao.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Naomba kwa ruhusa yako, kuwapongeza wahitimu wote utakaowatunuku vyeti vyao leo hii. Ikumbukwe kuwa jitihada zao katika mafunzo, nidhamu na kuwa na malengo ndivyo vimekuwa nguzo kuu katika kufaulu na kuhitimu mitihani hii ya kitaaluma.

Kwa wale wote ambao hawajamaliza mitihani yao kwa sababu anuai, napenda kuwatia moyo kuendelea kuongeza bidii nao wakati kama huu mwakani waweze kuhitimu na kutujumuisha tena katika tukio la kitaaluma kama hili na hatimaye kutunukiwa vyeti kama wenzao wanavyo pata hii leo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Pamoja na sifa za kitaaluma watakazopata wahitimu wetu leo na ili wafanye kazi za ununuzi na ugavi kwa mujibu wa Sheria, wanatakiwa wajisajili na Bodi kwenye mojawapo ya ngazi za usajili kitaaluma kuanzia ‘’*Technician Category, ‘’Graduate’’ na ‘’Approved Category’’ kwa Wahitimu wa CPSP-T na kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kukua kitaaluma ili hatimaye waweze kuwa wabobevu kitaaluma na kuomba kusajiliwa kwenye ngazi ya ‘’Authorized Category’’.*

**Mhesimiwa Mgeni Rasmi**

Naomba uniruhusu nitaje mambo machache ambayo Bodi hii imeendelea kuyafanya chini ya miongozo ya Wizara yako katika eneo la mafunzo na mitihani:

(a) Bodi imepitia na kupendekeza kuidhinishwa kwa mitaala ya vyuo vya elimu ya juu vitatu vinavyotoa mafunzo ya fani ya ununuzi na ugavi, vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino - Mwanza (SAUT-Mwanza), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Chuo

Kikuu cha Uislam-Morogoro, na Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo, Dodoma.

(b) Kuendesha Mafunzo Endelevu ya Kitaalamu - Continued Professional Development (CPD) Training kupitia Semina za kila Mwezi, mafunzo kulingana na mahitaji ya taasisi na wataalam yaani tailarmade training.

(c) Bodi imefanikiwa kuendesha mafunzo mahususi ya kitaaluma ya ukaguzi yaani Specialized training program for Procurement and Supply Auditors in auditing skills and methodology. Tunaamini mafunzo haya yatawasaidia wataalam wa ununuzi kuwajengea uwezo katika eneo la ukaguzi hivyo kuimarisha weledi wao kiutendaji, kutumika katika ukaguzi kwenye eneo la ununuzi na ugavi na kupanua wigo wa utaalumu wa ukaguzi na njia zake za ukaguzi kwa wataalum wabobevu katika taaluma ya ununuzi na ugavi inchini.

(d) Bodi imeendeleza mashirikiano na taasisi za nje kama vile "*International Federation of Purchasing and Supply Management (IFPSM)" ili kuendelea kukuza viwango vya*

*ubora kitaaluma na kuwafanya wahitimu hawa kuendelea kukubalika kimataifa.*

(e) Bodi imeendelea kusajili wataalam wa ununuzi na ugavi na kusimamia miongozo ya Maadili ya kitaalamu kwa wataalam wake na hata leo wahitimu wa cheti cha CPSP wataapa kama ishara ya kukubali kuitumikia taaluma wanayoipata kuzingatia muongozo ya maadili kitaaluma na weledi ili kuleta maendeleo kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

(f) Bodi imeendelea kulea vyama vya wanafunzi wanaosoma kozi za Ununuzi na Ugavi nchini kwa lengo la kuwajengea dhana ya maadili kitaaluma na uongozi toka wakiwa bado vyuoni. Sambamba na hili, tumeendelea kufanya mikutano kwa wanafunzi wa fani ya ununuzi na ugavi kushirikiana na vyuo vyao ili kuhamasisha maadili na weledi katika taaluma hii.

(g) Kwa Mwaka huu wa fedha, Bodi imeendesha mashauri ya kinidhamu kwa wataalam wa ununuzi na ugavi wapatao 15 na kutoa adhabu mbalimbali ili kuendelea

kulinda weledi kitaaluma katika utendaji wa mnyororo wa ununuzi na ugavi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Pamoja na majukumu ya Bodi bado niruhusu niseme kwa ufupi kuhusu changamoto zilizopo zinazoikabili Bodi hii;

(a) Kuwepo kwa waajiri wanaojiri wataalamu wasiosajiliwa na Bodi katika baadhi ya taasisi binafsi kinyume na matakwa ya sharia iliyoanzisha Bodi hii yaani '*'PSPTB Act, CAP 179*''.

(b) Kuwatumia wataaluma wasio na sifa kuongoza vitengo vya ununuzi na ugavi, kinyume na kanuni za Bodi na waraka No. 3 wa ofisi ya Rais Utumishi kwa kada zilizoko chini ya wizara yako hii ya fedha. Kwani waraka huu pamoja na muongozo wa usajili wa Bodi hii, unataka Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi awe amesajiliwa na PSPTB katika ngazi ya Authorized Category ili kuwa na wataalum wenye uzoefu na sifa stahiki za kusimamia utendaji wa mnyororo wa ununuzi na ugavi.

(c) Kuwepo kwa wadau mbalimbali wanaoingilia michakato ya ununuzi na ugavi, hivyo, kudhoofisha utendaji wa wataalamu waliosajiliwa kufanya kazi zao kwa mujibu wa elimu, taaluma, sheria na muongozo mbali mbali. Hii imepelekea watu nje ya taaluma kuwa kama wakuu wa vitengo vya ununuzi na kuendelea kufanya kazi za ununuzi na ugavi pasipo kusajiliwa na Bodi kinyume na kifungu cha 12 na 47 cha Sheria ya PSPTB, Sura 179.

(d) Ufinyu wa bajeti katika kutekeleza majukumu yake haswa katika eneo la kusimamia na kuendesha mashtaka ya kimaadili, ukaguzi wa ukidhi wa sharia ya PSPTB kwa watendaji wa mnyororo wa ununuzi na ugavi katika sekta ya umma na sekta binafsi kama hitaji la kisheria na kutokuwa na uwezo wa kundelea na ujenzi wa jengo la PSPTB katika kiwanja cha Medeli kutumia mapato yake.

(e) Baadhi ya Maafisa Masuuli “Accounting Officers” kushindwa kufadhili mafunzo ya kuwajengea weledi watumishi wao wa kada ya Ununuzi na Ugavi na kupelekea wataalam kutokidhi pointi 40 za mafunzo ya kitaaluma kulingana na kanuni na sera ya mafunzo ya

PSPTB. Kadhia inafanya wataalumu kushindwa kuendana na mabadiko ya kitaaluma na kiutendaji katika mnyororo wa ununuzi na ugavi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Niruhusu niwapongeze na kuwashukuru wakufunzi na wahadhiri kutoka vituo mbalimbali vya mafunzo ya kitaaluma na vyuo vikuu nchini waliotumia muda wao, taaluma zao, maarifa na weledi wao katika kuwaelimisha watahiniwa wa mitihani ya Bodi hii na kufanikisha kuweza kufaulu mitihani hii ya kitaaluma na hatimae kutujumuisha leo katika mahafali hii.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB **Ndugu Jacob J. Kibona** ili aseme aliyonayo kwa ajili ya hafla hii na kisha akukaribishe rasmi ili uzungumze na halaiki hii ya kitaaluma.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza.**